






# MALKIA NYUKI

## JARIDA LA KAMPASI YA MIZENGO PINDA

## CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

## 2024

Issue 1, Volume 2
December 2024




**YALIYOMO.........................................................................................Uk**

Ujumbe Kutoka Kwa Kaimu Rasi Wa Kampasi ya Mizengo Pinda..........................................01

WAJUMBE WA BODI YA NDAKI..........................................................................................02

UONGOZI WA CHUO..........................................................................................................03

Mtambue Mdudu Nyuki na Faida Zake.................................................................................04

Safari ya Mhitimu wa SUA Kueleke Ujasiriamali wa Bidhaa Zitokanazo na Rasilimali Nyuki...........................................................................................................09

SUA Kampasi ya Mizengo Pinda yashiriki vyema kwenye Maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika Mkoani Dodoma na kufungwa na Makamu wa Raisi wa Jamahuri ya Muungano Wa Tanzania Dkt Phipo Mpango tarehe 20 Mei 2024....................................10

Watafiti na Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kuzitafsiri kwa vitendo tafiti mbalimbali wanazozifanya ili ziwe na maana kwa wananchi....................................12

Mhe. Dkt. Doto Biteko Atangaza Maagizo Mapya kwa Wizara na Mikoa Kukuza Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi..........................................................................................13

Jinsi Mradi wa Elimu ya Juu Unavyochochea Maendeleo ya SUA Kampasi ya Mizengo Pinda.........................................................................................................16

Kaimu Rasi wa Ndaki, Prof. Anna Sikira, Atoa Mwongozo kwa Wanachuo Wapya Kampasi ya Mizengo Pinda.........................................................................................18

MPC-Katika Michezo..........................................................................................................19

# Ujumbe Kutoka Kwa Kaimu Rasi Wa Kampasi ya Mizengo Pinda



**Prof. Anna Sikira**

Mpendwa Msomaji, Napenda kukukaribisha kwenye toleo letu la Pili la MALKIA NYUKI Jarida la Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo Kampasi ya Mizengo Pinda kwa mwaka 2024. Jarida letu linaelezea mambo mbalimbali yanayofanywa na kampasi yetu kama ifatavyo,
Kampasi inatekeleza majukumu makuu matatu kama zilivyo taasisi nyingine zote za elimu ya juu nchini ambayo ni kufundisha, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na uzalishaji mali katika nyanja za kilimo, mifugo, maliasili na utalii.

Kampasi kwa sasa inaendesha programu tatu, moja ikiwa ni ya Shahada ya awali katika Usimamizi wa rasilimali nyuki, programu ya pili ni Stashahada katika Uzalishaji na usimamizi wa mazao na programu ya tatu ni ya Astashahada katika Uongozaji Watalii na Uwindaji wa Kitalii.
Mbali na kufundisha, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na uzalishaji mali katika nyanja za kilimo, mifugo, maliasili na utalii.pia watumishi na wanachuo ushiriki katika mambo mbalimbali ya kijamii kama kuchangia damu,michezo,maonesho ya nanenane,maonesho ya nyuki,wiki ya mwanakatavi na kushiriki katika makongamano na warsha yanayoratibiwa na Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Mizengo Pinda kwa kushirikiana na mikoa,wilaya na halimashauri zake za Nyanda za Juu Kusini katika kujengeana huwezo.

Kampasi ya Mizengo Pinda imelenga kuboresha mitaala yake kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa Elimu katika kuboresha mitaala hiyo,Mbali na mitaala Kampasi ya Mizengo Pinda imelenga kuboresha miundo mbinu yake kupitia Mradi wa Elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi (HEET), ambpo Kampasi ya Mizengo Pinda itajengewa majengo mawili, Jengo la Taaluma na Bwalo.
Napenda kumshuku Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha vyuo kimkakati vyenye kuleta mageuzi ya kiuchumi katika sekta ya Elimu na Kilimo kwa maendeleo ya nchi yetu.
Kupitia chuo chetu kinasaidia kuleta mageuzi ya kiuchumi katika mikoa ya nyanda za juu kusini katika kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na uzalishaji mali katika nyanja za kilimo, mifugo, maliasili na utalii.
Nawatakia kila la kheri.

PROF. ANNA SIKIRA
Kaimu Rasi Kampasi ya Mizengo Pinda-Katavi

# WAJUMBE WA BODI YA NDAKI



**Dkt. Tulole Lugendo Bucheyeki**
Mwenyekiti



**Dkt. Hellena M. Mushi**
Mjumbe



**Prof. Anna Sikira**
Katibu



**Daniel Sirira**
Mjumbe



**Naftal Mahewa**
Mjumbe



**SACC. Ebrantino E. Mgiye**
Mjumbe



**Mussa P. Ng’hwani**
Mjumbe

# UONGOZI WA CHUO
# KAMPASI YA MIZENGO PINDA



## Prof.Anna N. Sikira

Kaimu Rasi wa Ndaki

Associate Professor in Development and Strategic Studies
Email: sikira@sua.ac.tz
Phone: +255 252955233



## Prof.Jeremiah R.Makindara

Kaimu Naibu Rasi wa Ndaki-Utawala, Mipango na Fedha

Associate Professor of Business Management
Email: makj@sua.ac.tz
Phone: +255 252955234



Nyuki ni wadudu wanaoishi kwa makundi, ambapo ukubwa wa kundi moja la nyuki unatofautiana, kuanzia maelfu machache hadi maelfu mengi kufikia 60,000. Mwili wa nyuki umegawanyika katika sehemu tatu,  kichwa, kifua, na tumbo. Wana miguu sita na vipapasio viwili kama wadudu wengine. Tofauti na wadudu wengine, nyuki wana tabia ya kutengeneza masega na kuhifadhi asali na chavua katika seli za masega.

## Aina za nyuki

Kuna aina tofauti za nyuki zaidi ya 20,000 duniani ambazo hutofautishwa kwa ukubwa wa miili yao na tabia. Chini ya asilimia 4 ya nyuki wote ndio wanaozalisha asali, na siyo nyuki wote wana uwezo wa kuzalisha asali, Pia kuna aina kuu mbili za nyuki, nyuki wanaodunga na nyuki wasiodunga.

## Jinsia za Nyuki na Majukumu Yao

Kundi la nyuki linaundwa na nyuki wa jinsia mbili:

I. Majike

- Malkia, Anamajukumu ya kuongoza kundi na kutaga mayai. Malkia ndiye nyuki mkubwa zaidi katika kundi, na maisha yake yote yanahusisha kuhakikisha uendelevu wa jamii ya nyuki.
- Vibarua, Hawa ni nyuki wa kike walio wengi katika kundi. Wanawajibika kwa kazi mbalimbali kama vile kukusanya chakula (nectar na chavua), kujenga na kutunza masega, na kuwahudumia watoto wa nyuki.

II. Madume

- Madume (Drones), Wanawajibika kwa kazi moja kuu kupandana na malkia. Madume hawana uwezo wa kucha kucha kazi za kutunza masega au kukusanya chakula. Baada ya msimu wa kupandana, wengi wao hufariki.

## Majukumu ya Malkia

i. **Mama wa Kundi,** Malkia ndiye mama wa kundi la nyuki, akihakikisha uendelevu wa kundi kwa kutaga mayai.Malkia anataga mayai na anaweza kuishi kwenye mzinga kwa muda wa miaka 3-5.

ii. **Lishe:** Malkia analishwa maziwa ya nyuki (royal jelly) ambayo ni lishe maalum inayompa nguvu na uwezo wa kuendelea kutaga mayai.

iii. **Feromoni,** Malkia huzalisha feromoni, ambazo mara nyingi hujulikana kama “harufu ya malkia.” Feromoni hizi husaidia kudhibiti tabia za nyuki katika mzinga na kuhakikisha mshikamano na utulivu wa kundi.

## Majukumu ya Vibarua

i. **Kupasha Joto Majana:** Vibarua hupasha joto majana (mayai, mabuu, na pupa) na kufanya usafi katika seli za masega.

ii. **Kulisha Majana na Malkia:** Wanawajibika kulisha majana (mayai, mabuu) na malkia

**iv. Kudhibiti Joto la Mzinga:** Wanaruhusu au kuziba njia za hewa ili kurekebisha kiwango cha joto kinachostahili ndani ya mzinga, kuhakikisha mazingira bora kwa nyuki wote.
**v. Usafi wa Mzinga:** Kazi yao ni kuweka mzinga safi, kuondoa uchafu na vitu visivyohitajika.
**vi. Utunzaji wa Chavua na Kutengeneza Asali:** Wanatunza chavua katika seli na hubadilisha mbochi kuwa asali kwa shughuli ya uvukizi.
**vii. Ulinzi wa Mzinga:** Wanakulinda sehemu ya kuingilia kwenye mzinga dhidi ya wavamizi na hatari zozote.
**viii. Ukusanyaji wa Rasilimali:** Vibarua hukusanya mbochi, chavua, maji, na malighafi nyingine kutoka kwenye miti mbalimbali ili kutengeneza gundi (plant resins).
**ix. Utengenezaji wa Maziwa ya Nyuki:** Wanahusika katika utengenezaji wa maziwa ya nyuki (royal jelly) ambayo hutumika kulisha malkia na majana.

## Majukumu ya Madume

Madume wanajukumu moja kuu ambalo ni kujamiana na malkia. Hawashiriki katika kazi za ujamaa wa kundi la nyuki.

## Tabia za Nyuki na Shughuli zinazofanywa na nyuki

**i. Kulishana**, Nyuki hulishana kwa kutumia nectar na chavua zilizokusanywa.
**ii. Kusafishana,** Nyuki hushirikiana kusafishana miili yao ili kudumisha usafi wa kundi.
**iii. Kupigana/Kulinda Maadui,** Nyuki hulinda mzinga wao dhidi ya wavamizi kwa kutumia mbinu mbalimbali za kujilinda.
**iv. Kusafisha Mzinga,** Wanafanya usafi ndani ya mzinga, kuondoa uchafu na vitu visivyohitajika.
**v. Kutafuta Chakula,** Nyuki hukusanya nectar, chavua, maji, na resin kutoka kwenye miti ili kutengeneza chakula na gundi.
**vi. Kuzaliana,** Nyuki wanazaliana ili kuhakikisha uendelevu wa jamii yao.
**vii. Kupotea Njia,** Wakati mwingine nyuki wanaweza kupotea njia, hasa wanapotafuta chakula au makazi mapya.
**viii. Kuibiana Chakula,** Wanaweza kuiba chavua na nectar kutoka kwenye mzinga mwingine ikiwa chakula ni kidogo.
**ix. Kupepea (Feni),** Nyuki hutumia mbawa zao kupepea hewa ili kudhibiti joto la mzinga.
**x. Kuwasiliana,** Nyuki hutumia njia mbili kuu za mawasiliano:
a) Kuwasiliana Kimwili, Nyuki hutumia miili yao kuwasiliana kupitia michezo maalum. Kuna aina mbili za michezo:
• Mchezo wa Mduara, Huonesha eneo na umbali wa makazi mapya.
• Mchezo wa Kuonesha Eneo (Waggle), Huonesha eneo, umbali na kiwango cha mbochi inayopatikana sehemu fulani.
b) Kuwasiliana kwa Kutumia Kemikali,
• Kemikali ya Kuwashitua, Inatumika kutaarifiana kuhusu uwepo wa adui. Hii ndio sababu moshi hutumika kupoza nyuki.
• Kemikali Elekezi, Inatolewa na nyuki mmoja kuelekeza wengine kwenye makazi au sehemu yenye chakula.
• Kemikali ya Malkia, Inaendesha shughuli zote kwenye kundi la nyuki.
• Kemikali ya Watoto, Inahamasisha vibarua kutafuta chakula.
**xi. Kutambua Sehemu,** Nyuki wana uwezo wa kutambua sehemu mbalimbali, kukumbuka makazi yao na vyanzo vya chakula.
**xii. Kufautisha Rangi,** Harufu na Radha: Wana uwezo wa kutofautisha rangi, harufu, na radha za maua mbalimbali.
**xiii. Upendeleo wa Maua,** Nyuki wanapendelea kutembelea aina moja ya maua hadi yatakapoisha ndipo huama.

**xiv. Kuhama kwa Makundi,** Nyuki wanahama kutoka katika mzinga kutokana na hali mbaya ya mazingira ili kuhakikisha uendelevu wa kundi.
**xv. Kuhama kwa Njia ya Kujigawa:** Kuhama kwa makundi ya nyuki kwa njia ya kujigawa ni njia ya kuhakikisha kuwa lengo la kuendeleza kizazi linatimizwa.

## Mambo yanayosababisha nyuki kuhama

**Utashi wa Asili,** Nyuki wana utashi wa asili wa kutaka kuongezeka na kuzaliana.
Uhaba wa Chakula, Ukosefu wa chakula unaweza kusababisha nyuki kuhama kutafuta eneo lenye chakula zaidi.
**Nafasi Ndogo,** Nafasi ndani ya mzinga inapokuwa ndogo mno, inawazuia nyuki wafanyakazi kutekeleza majukumu muhimu kama kujenga masega, kuweka akiba ya asali, na kulea watoto.
**Maadui wa Nyuki,** Uwepo wa maadui wanaovamia mzinga unaweza kuwalazimisha nyuki kuhama.
**Madawa ya Kilimo,** Matumizi ya madawa ya kilimo ambayo huwadhuru nyuki yanaweza kusababisha kuhama kwao.
**Hali ya Hewa,** Hali mbaya ya hewa kama joto kali, baridi kali, unyevu mwingi, na mvua nyingi inaweza kuwafanya nyuki kuhama.
**Uvunaji Usiozingatia Kanuni Bora,** Uvunaji mbaya kama kuvuna masega yote bila kuwaachia nyuki asali, unaweza kusababisha nyuki kuhama.

## Aina za Makundi Yanayohama

**Kundi linalohama Kutokana na Hali ya Mazingira;** Kundi la aina hii huhama kutokana na kukosa usalama, kusumbuliwa na maadui, au hali mbaya ya hewa kama joto kali, baridi kali, au mvua nyingi.
**Kundi linalohama kwa Ajili ya Kutafuta Chakula;** Nyuki huhama na kwenda sehemu nzuri ili kutafuta chakula cha kutosha.
**Kundi linalohama kwa Ajili ya Kujiongeza;** Kundi la aina hii huhama kutoka kwenye mzinga kwa madhumuni ya kuongezeka. Ufikiapo msimu wa asali, nyuki huzaliana kwa wingi hivyo nafasi kwenye mzinga huwa haitoshi na nyuki huamua kujigawa. Kundi hili ni tofauti na makundi mawili ya mwanzo kwa sababu halihami lote ila hujigawa, ambapo sehemu moja ya kundi huhama na kuacha sehemu nyingine ndani ya mzinga.

## Jinsi ya kuzuia kujigawa kwa Nyuki

Mfugaji nyuki anawajibika kufanya uchunguzi mara kwa mara ili kugundua dalili za nyuki kuhama na kuwazuia wasihame. Kuna njia mbili za msingi za kuzuia kujigawa kwa nyuki:
**i. Kuzuia Kitendo cha Kujigawa;** Wakati wa ukaguzi wa mzinga, ukikuta nyuki wametengeneza vyumba vya malkia, viharibu mara moja au jitahidi kuwagawa mwenyewe.
**ii. Kuzuia Sababu za Kujigawa;** Hakikisha unawapa nyuki chakula wakati wa uhaba wa chakula na kuwalinda dhidi ya maadui kwa kukagua na kusafisha mzinga mara kwa mara.

## Jinsi ya kuanza kufuga Nyuki

**Mahitaji ya Nyuki katika Mazingira na Uchaguzi wa Shamba la Nyuki (Manzuki).**
Nyuki, kama viumbe hai wengine, wanayo mahitaji muhimu katika mazingira yao. Moja ya nguzo muhimu katika ufugaji nyuki ni kuwa na shamba la nyuki (manzuki) linalofaa kwa ustawi wa nyuki. Mafanikio mazuri ya shughuli za ufugaji nyuki yanategemea hatua muhimu za kuanzisha na kusimamia manzuki.
Manzuki ni eneo maalum chini ya hekta 50 lenye makundi ya nyuki yanayomilikiwa au shamba linalotumika kuhifadhi makundi ya nyuki yaliyopo ndani ya mizinga kwa malengo ya kuzalisha mazao ya nyuki.

## Sifa za Manzuki

**Eneo la Chakula;** Eneo liwe na upatikanaji wa chakula (mbochi na chavua). Kwa kuzingatia shughuli wanazofanya nyuki, upatikanaji wa mbochi na chavua unatakiwa kuwa ndani ya kilometa 1 kutoka eneo la manzuki. Ikiwa ni umbali mrefu, nyuki wanachoka kusafiri umbali mrefu. Mimea mingi inayopendwa na nyuki inapaswa kuwa ndani ya kilometa 2 kutoka eneo la manzuki. Pia inashauriwa kuwa na mimea yenye utofauti wa msimu wa uchanuaji maua.

**Chanzo cha Maji;** Upatikanaji wa chanzo cha maji ndani ya umbali wa kilometa 2 kutoka eneo la manzuki. Inafaa zaidi kati ya nusu kipenyo cha mita 500.

**Umbali na Makazi ya Watu;** Eneo la manzuki linafaa kuwepo angalau umbali wa mita 500 kutoka makazi ya watu kama vile shule, soko, hospitali, au barabara kuu.

**Hatari za Mafuriko;** Kusiwe na uwezekano hatarishi mkubwa wa mafuriko.

Eneo Tambarare, Eneo linatakiwa kuwa tambarare au kutokuwa na mteremko mkali ili kurahisisha huduma.

**Athari za Hali ya Hewa;** Eneo lisiwe na athari kubwa za hali ya hewa kama joto kali, unyevunyevu, baridi kali, na upepo mkali.

**Kivuli na Kinga ya Upepo;** Eneo linatakiwa kuwa na kivuli cha kutosha na mimea ya kukinga upepo.

**Urahisi wa Kufikika;** Eneo liwe rahisi kufikika.

**Mzingato wa Mizinga;** Kusiwe na mlundiko mkubwa wa mizinga katika sehemu moja ili kuepuka nyuki kuibiana asali na baadhi ya mizinga kukosa makundi ya nyuki kwa muda mrefu.

**Viuatilifu;** Eneo liwe mbali na sehemu inayotumia kilimo cha viuatilifu, mfano tumbaku. Umbali wa kilometa 5-7 ndio umbali wa nyuki kuruka.

**Athari za Mot;** Eneo lisiwe na athari za moto.

**Ulinzi;** Eneo linahitaji kuwa na ulinzi.

**Kinga Dhidi ya Maadui;** Hakikisha kuna kinga dhidi ya maadui wa nyuki kama nyegere, siafu, au mifugo.

## Aina za Manzuki

Tanzania kuna aina kuu tano za manzuki:

**Manzuki ya Juu ya Miti;** Hii ni manzuki ambapo mizinga ya nyuki hutundikwa kwenye matawi ya miti mirefu. Hutumika kufuga nyuki wanaouma na hutumika zaidi kwenye misitu ya miombo.

**Manzuki ya Jukwaa au Vichanja;** Katika aina hii ya manzuki, mizinga huwekwa juu ya majukwaa yenye kimo cha mita 1.2 kutoka usawa wa ardhi. Hutumika kwenye mashamba madogo madogo na makubwa ya miti na maeneo yenye mbuga za nyasi.

**Manzuki ya Viota vya Asili;** Hii ni manzuki ambapo mfugaji nyuki hufanya marekebisho kwenye mapango ya asili kwenye miti na ardhini ambamo nyuki hufanya makazi yao. Hutumika zaidi na jamii ya wandorobo katika wilaya ya Simanjiro, Manyara.

**Manzuki ya Ndani ya Nyumba;** Katika aina hii, mizinga ya nyuki huwekwa kwenye majukwaa yenye kimo cha mita 1.2 ndani ya nyumba maalum yenye matundu ukutani. Matundu haya huwezesha kuingia na kutoka kwa urahisi.

**Manzuki ya Michirizi au Paa ya Nyumba;** Hii ni manzuki ambapo mizinga ya nyuki huwekwa kwenye michirizi ya nyumba za kuishi. Inafaa kwa ufugaji wa nyuki wasiouma. Hii aina ya manzuki inamwezesha mfugaji nyuki kuwalinda nyuki dhidi ya wezi na maadui.

Usimamizi wa Manzuki

Mafanikio ya ufugaji nyuki hutokana na usimamizi makini wa manzuki. Mfugaji nyuki anatakiwa kufuata hatua maalum ili kupata matunda bora ya kazi yake, Ni muhimu kuzingatia kanuni zifuatazo ili kufanikisha shughuli za ufugaji nyuki:

**Kuwa na Makundi Yenye Uwezo;** Hakikisha unakuwa na makundi ya nyuki yenye uwezo na yanayotokana na ukoo wa nyuki wenye juhudi.

**Ukaguzi wa Makundi;** Fanya ukaguzi wa makundi ya nyuki mara kwa mara ili kufahamu

maendeleo ya kila kundi
**Kuunganisha Makundi Dhaifu;** Unganisha makundi ya nyuki dhaifu ili kuunda makundi makubwa yanayoweza kuzalisha asali kwa wingi.
**Matumizi ya Vifaa vya Kinga;** Tumia mavazi ya kinga na bomba la moshi kwa utaratibu wakati wa kukagua makundi ya nyuki na kurina asali.
**Kumbukumbu za Kila Kundi;** Tunza kumbukumbu ya kila kundi ili kujua ni lini lilipatikana, tabia ya nyuki wake, na uzalishaji wake kwa msimu.
**Matengenezo ya Mizinga;** Fanya matengenezo ya mizinga mibovu na udhibiti maadui wa nyuki mara kwa mara.

# Safari ya Mhitimu wa SUA Kuelekea Ujasiriamali wa Bidhaa Zitokanazo na Rasilimali Nyuki.




Dwasi Denis Johnson, ni mhitimu wa Shahada ya Sayansi ya Awali ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki katika chuo kikuu cha kilimo cha Sokoine Kampasi ya Mizengo Pinda. Anatumia ujasiriamali wa bidhaa zitokanazo na rasilimali nyuki, kama asali ya nyuki wakubwa na wadogo, pia anaonyesha bidhaazake katika maonesho mbalimbali kama maonesho ya Wiki ya Mwanakatavi ambayo hufanyika kila mwaka mkoani Katavi kwa lengo la kuwakutanisha wajasiriamali, taasisi, wakulima, wafugaji na kutangaza utalii na fursa zote zipatikanazo katika mkoa wa Katavi, maoneho ya nane nane na maonesho mengine mengi yanayohusiana na hayo.






*Katika picha: Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Rungwa pamoja na watu wengine wakipata elimu kuhusu uzalishaji wa asali kupitia mdudu nyuki na kalenda sahihi ya uandaaji wa mizinga katika banda la Halmashauri ya Mpimbwe katika Maonesho ya Wiki ya Mwanakatavi.*

Bw. Dwasi amemshukuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mpimbwe, Bi. Shamimu Mwariko, kwa kuendelea kuwapa ushirikiano kama wajasiriamali wa Halmashauri ya Mpimbwe.

Kwa sasa, Bw. Dwasi ana mizinga ishirini (20) iliyopo kwenye kijiji cha Kanindi, yenye uwezo wa kutoa lita 15 hadi 20 za asali. Hivyo, Bw. Dwasi anawaomba wadau ambao wanaweza kumsaidia kupata mizinga ya kisasa inayogharimu kiasi cha shilingi milioni mbili (2,000,000) ili aweze kuzalisha zaidi asali.

# SUA Kampasi ya Mizngo Pinda yashiriki vyema kwenye Maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika Mkoani Dodoma na kufungwa na Makamu wa Raisi wa Jamahuri ya Muungano Wa Tanzania Dkt Phipo Mpango tarehe 20 Mei 2024




Daktari Philipo Mpango, Makamu wa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,amekabidhiwa Tuzo na Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki kwa ajili ya kutambua mchango wa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Daktari Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza sekta ya Ufugaji Nyuki na Uhifadhi wa mazingira Nchini.
Tuzo hiyo imetolewa wakati wa Maadhimisho ya siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika kitaifa Mkoani Dododma katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Tarehe 20 mei 2024.
Katika Maadhimisho hayo Makamu wa Raisi Daktari Philipo Mpango ametoa Rai kwa wote wenye dhamana ya kusimamia maeneo yaliyoifadhiwa kwa kuyalinda na kuyaendeleza maeneo hayo ili yasiaribiwe na shuguli za kibanadamu.
Pia Makamu wa Raisi ameitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana na wadau katika kutoa elimu kwa wafugaji nyuki ili waweze kufuga kitaalam kwa kutumia vifaa sahihi vitakavyoongeza kiwango cha uzalishaji na ufugaji wenye tija.

Miongoni wa wadau waliotajwa na makamu wa Raisi, pamoja na Chuo Kikuu Cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda ambao wanatoa Shaada ya awali ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki kwa kuwatumia walaamu kutoka katika chuo hicho ili kutoa elimu kwa wafugaji wa Nyuki na kuongeza Uzalishaji kwa wafugaji hao. Mbali na Chuo kikuuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Pia Makamu wa Raisi amevitaka Vyuo vya Ufundi stadi (VETA) vilivyopo kwenye maeneo rafiki ya ufugaji nyuki kuanzisha kozi hizo na uchakataji wa mazao yatokanayo na nyuki.
Kwa Upande wa Waziri wa Maliasili na Utalii Angellah Kairuki amesema Wizara itaendelea kushirikiana na wadau ili kuongeza kasi ya Ufugaji Nyuki na kuhakikisha Uzalishaji wa Asali Unaongezeka Kutoka Tani 32671 sasa na kufikia Tani 138000 ifikapo 2024.

Waziri amesema Wizara itaongeza uzalishaji wa Chavua, kuhamasisha na kuongeza idadi ya mizinga, kuongeza Uzalishaji wa Asali ya Nyuki wasiodunga, na kuongeza dhamani ya aina sita ya mazao ya Nyuki kwa kutumia mazao mengine, kama sumu ya Nyuki, Gundi ya Nyuki.

Pia Waziri amesema Wizara itawajengea Uwezo wadau na watalaam ili waweze kufanya kazi Zaidi pamoja na kutenga fedha na kuhakikisha vitendea kazi na miundo mbinu vinaimarishwa katika maeneo ya kufugia Nyuki.

*Katika picha ni baadhi ya wadau waliojitokeza katika maadhimisho ya siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Mkoani Dodoma na kufika katika banda la Chuo Kikuuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Na kupata maelezo ya matumizi ya Mashine ya kukamulia Asali kutoka kwa Prosper Mahenge,mwanafunzi wa mwaka wa pili aanayesoma Shaada ya awali ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki katika Kampasi ya Mizengo Pinda iliyopo Mkoani Katavi*







## Watafiti na Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kuzitafsiri kwa vitendo tafiti mbalimbali wanazozifanya ili ziwe na maana kwa wananchi.




*Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Mhe. Jamila Yusuph akiwa katika Banda la SUA katika maonesho ya sikukuu ya wakulima (NANENANE), wafugaji na wavuvi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Viwanja vya John Mwakangale vilivyopo Jijini Mbeya.*

Watafiti na Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wametakiwa kuzitafsiri kwa vitendo tafiti mbalimbali wanazozifanya ili ziwe na maana kwa wananchi ambao wanaitazama SUA kama chemchem ya maarifa na ujuzi wa teknolojia mbalimbali za kilimo, ufugaji na uvuvi
wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Mhe. Jamila Yusuph alipokuwa akitembelea Banda la SUA katika maonesho ya sikukuu ya wakulima (NANENANE), wafugaji na wavuvi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale vilivyopo Jijini Mbeya, ambapo ameeleza kuwa SUA imekuwa ikifanya tafiti nyingi nzuri lakini kama hazitawafikia wananchi katika njia rahisi zitapoteza maana.

Mhe. Jamila amesema hayo baada ya kuelezwa na watafiti wa Kampasi ya Mizengo Pinda (SUA) kuhusu njia za kisasa za utengenezaji wa mizinga ya nyuki, urinaji wa asali pamoja na kulima kilimo cha alizeti kwa tija kulingana na tafiti zilizofanyika katika udongo wa mikoa ya nyanda za juu kusini.
Amesema tafiti hizo na nyingine zinatakiwa wananchi wazifahamu na wazitumie ili wafanye shughuli zao kwa tija kwa kukuza uchumi binafsi na taifa kwa ujumla.

**“Nimeona mnafanya kazi nzuri sana za tafiti, lakini tujitahidi zifike kwa wananchi, wazielewe kisha wazitumie kwa manufaa yao. Hii itasaidia kuinua shughuli za kilimo kwani watakuwa wanatumia teknolojia za kisasa zilizothibitishwa kupitia tafiti zenu”**, alisema Mhe. Jamila.

# Mhe. Dkt. Doto Biteko Atangaza Maagizo Mapya kwa Wizara na Mikoa Kukuza Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, akizungumza wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya sherehe za maonesho ya Nanenane jijini Mbeya*

Agosti 2, 2024, Mbeya - Katika ufunguzi wa Sherehe za Maonesho ya Wakulima, Wafugaji, na Wavuvi ya Nanenane, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, ametoa maagizo matano kwa Wizara ya Kilimo, Taasisi, na Mikoa ili kukuza na kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo, na uvuvi nchini. Maagizo hayo yametolewa Agosti 2, 2024, jijini Mbeya, katika ufunguzi wa Sherehe za Maonesho ya Nanenane kwenye Viwanja vya John Mwakangale.

Dkt. Biteko amesisitiza umuhimu wa mipango bora ya matumizi ya ardhi, akizingatia mifugo iliyoingizwa katika mikoa ya nyanda za juu kusini ambayo inaweza kuathiri mazingira. Amezitaka Wizara zote husika na Wakuu wa Mikoa kuchukua hatua stahiki kukabiliana na matumizi mabaya ya viuatilifu na kemikali, ambazo zinaathiri afya ya binadamu, viumbe hai vingine, an mazingira. Pia amehimiza umuhimu wa kuhifadhi chakula kwa matumizi ya baadaye na kutotumia mazao ya biashara kabla ya kukomaa ili kulinda soko la ndani na nje.

Kuhusu maeneo ya taasisi za utafiti wa kilimo, Dkt. Biteko amesisitiza kuwa yapewe hati miliki na yalindwe kwa madhumuni ya uzalishaji wa mbegu. Ameagiza Mamlaka husika kupima na kutenga ardhi kwa ajili ya kuzalisha mbegu na kuyalinda dhidi ya uvamizi. Aidha, kuhusu uhaba wa mbegu bora za malisho na mifugo, pamoja na vifaranga vya samaki, ameitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha upatikanaji wake unakuwa wa gharama nafuu.

Dkt. Biteko alibainisha ongezeko la asilimia 15 la uzalishaji wa mazao ya chakula katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutoka tani 11,814,480.63 mwaka 2022/2023 hadi tani 13,559,101.43 mwaka 2023/2024. Amesema, serikali imeweka jitihada kubwa katika kuhakikisha tija inaongezeka katika sekta ya kilimo kupitia Mpango wa Ruzuku ya Mbolea. Pia amesisitiza serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoka Shilingi 275 bilioni mwaka 2021/2022 hadi Shilingi 295 bilioni mwaka 2023/2024, na ya Wizara ya Kilimo kutoka Shilingi 294,162,071,000 kwa mwaka 2021/2022 hadi Shilingi 1.3 trilioni mwaka 2024/2025.



*Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde akizungumza wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya sherehe za maonesho ya Nanenane jijini Mbeya*

Kwa upande wa bei ya mahindi, Dkt. Biteko ameitaka Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula (NFRA) kusimamia utekelezaji wa agizo la Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha bei ya mahindi kwa kilo moja inauzwa shilingi 700 kama ilivyoombwa na wananchi. Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji na kuhimiza matumizi ya mbolea kupitia Mpango wa Ruzuku ili kuongeza tija na uzalishaji, ambapo matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani 313,593 mwaka 2022/2023 hadi tani 412,859.76 mwaka 2023/2024.

Dkt. Biteko ameishukuru Benki ya Azania na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kutoa mikopo kwa wakulima na kuwaomba kuongeza kasi ya kutoa mikopo nafuu kwa wakulima nchini. Katika maadhimisho hayo yenye kaulimbiu, "Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo, na Uvuvi," ililenga kuwakumbusha wananchi kuchagua viongozi bora katika uchaguzi wa 2024, hasa kwa kuzingatia kuwa shughuli za uzalishaji katika sekta za kilimo zinafanyika katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

Katika ufunguzi wa maonyesho hayo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Akson, amemshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha

kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali mkoani humo, ikiwemo ujenzi wa shule, vituo vya afya, na barabara.

Pia Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde, amesema Wizara ya Kilimo imeanza utekelezaji wa agizo la Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan la kutaka viwanja vya Nzuguni Dodoma na Uwanja wa John Mwakangale vijengwe ili kuwa na hadhi ya viwanja vya kimataifa vya maonesho ya Nanenane.

Katikita maonyesho hayo, wananchi walijitokeza kwa wingi katika banda la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda, iliyopo Mkoani Katavi, kujifunza na kujionea bidhaa zilizotengenezwa na wanafunzi. Kampasi ya Mizengo Pinda inatoa programu tatu, zikiwemo Shaada ya Sayansi ya Awali ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki, Stashaada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao, na Astashaada ya Uongozaji Watalii na Uwindaji wa Kitalii.



*mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda Mr Evaristus Magani akitoa elimu ya aina ya makundi ya nyuki na bidhaa zilizotengenezwa na wanafunzi wanaosoma Shaada ya Sayansi ya Awali ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki kwa wanafunzi mbalimbali waliotembelea bandani hapo katika maonesho ya nanenane ndani ya viwanja vya John Mwakangale Mkoani Mbeya.*



*Baadhi ya washiriki waliotembelea banda la SUA katika maonesho ya nanenane ndani ya viwanja vya John Mwakangale Mkoani Mbeya.*

## Jinsi Mradi wa Elimu ya Juu Unavyochochea Maendeleo ya SUA Kampasi ya Mizengo Pinda.



*Katika picha mwenye tai nyekundu: Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Raphael Chibunda, akitoa maelezo kwa mgeni rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mh. Mwanamvua Hoza Mrindo, na wageni mbalimbali walioudhuria sherehe hizo katika hafla ya utiaji saini wa ujenzi wa majengo mapya ya Kampasi ya Mizengo Pinda na Kampuni ya TIL CONSTRUCTION.*

Chuo kikuu cha kilimo cha Sokoine kimetiliana saini ya ujenzi wa majengo mapya ya Kampasi ya Mizengo Pinda na Kampuni ya TIL CONSTRUCTION, mradi wenye thamani ya shilingi bilioni 17.5 za Kitanzania.

Kupitia mradi huu, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kitajenga jumla ya majengo 9, ambapo majengo mawili yatajengwa katika Kampasi ya Solomon Mahlangu, majengo matano yatajengwa katika Kampasi ya Edward Moringe, na hapa Kampasi ya Mizengo Pinda yatajengwa majengo mawili.

Jengo la taaluma litakuwa na eneo la mita za mraba 5,840 na litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2000 kwa wakati mmoja, na jengo la pili ni hosteli yenye ukubwa wa mita za mraba 5,132 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 kwa wakati mmoja.

Mbali na majengo hayo, utajengwa mfumo wa maji taka pamoja na jengo litakalokuwa na vifaa vya kuzalishia, kuhifadhi, na kusambaza umeme, ikiwa ni pamoja na jenereta zinazotumika wakati wa dharura.



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Prof. Raphael Chibunda, na mwakilishi wa Kampuni ya TIL CONSTRUCTION wakisaini mkataba wa ujenzi wa majengo mapya ya Kampasi ya Mizengo Pinda ikishuhudiwa na viongozi mbalimbali wa serikali na pamoja na chama.*

Prof. Raphael Chibunda amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake binafsi za serikali ya awamu ya sita katika kuwezesha upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi wa kuendeleza sekta ya elimu ya juu nchini na kwa kuendelea kukiwezesha chuo kulipia gharama muhimu za uendeshaji wa chuo.

Vile vile, Prof. Chibunda ameishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiongozwa na Mh. Adolf

Faustine Mkenda (MB), Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mh. Omary Juma Kipanga (MB), na Prof. Crolyne Ignatus Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, pamoja na viongozi wengine wote wa wizara kwa misaada na miongozo wanayoipatia chuo na kukiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.



# Kaimu Rasi wa Ndaki, Prof. Anna Sikira, Atoa Mwongozo kwa Wanachuo Wapya Kampasi ya Mizengo Pinda.



*Kaimu Rasi wa Ndaki, Prof. Anna Sikira, akitoa Mwongozo kwa Wanachuo Wapya Kampasi ya Mizengo Pinda.*

Kaimu Rasi wa Ndaki, Prof. Anna Sikira, amewahimiza wanachuo wapya kujitambua na kufahamu kwamba lengo kuu la kuja katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ni kusoma. Alisisitiza umuhimu wa kujituma katika masomo na kushirikiana ili kufanikisha malengo yao ya kitaaluma.

Prof. Sikira pia aliwakumbusha wanachuo kulipa ada kwa wakati ili kuepuka usumbufu wakati wa mitihani. Aliongeza kuwa, wanachuo wanapaswa kutumia vyema ofisi za mshauri wa wanafunzi na ofisi nyinginezo za ndani ya chuo kwa ajili ya kupata msaada pale wanapokumbana na changamoto.

Katika mapokezi ya wanachuo wa mwaka wa kwanza, walikumbushwa umuhimu wa kuishi katika imani zao na kutenda matendo mema yanayompendeza Mwenyezi Mungu. Imam wa Msikiti wa Kibaoni, Shekhe Mwita Omari Salumu kutoka BAKWATA, pamoja na Frateri Augustine Mnyere kutoka TEC Parokia ya Usevya iliyopo kata ya Usevya, Halmashauri ya Mpimbwe, walitoa nasaha hizo kwa wanachuo.

Aidha, katika ukaribisho huo, vyombo mbalimbali na taasisi mbalimbali kama Takukuru, Bima ya Afya Taifa (NHIF), Uhamiaji, Polisi, na Dawati la Jinsia pia zilipata fursa ya kuzungumza na wanachuo wa mwaka wa kwanza.



*Baadhi ya wawakilishi wa Taasisi na Vyombo vya Ulinzi na Usalama, pamoja na baadhi ya wanachuo wa mwaka wa kwanza katika picha ya pamoja.*

# MPC-Katika Michezo

Chuo Kikuu Cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) Kampasi Ya Mizengo Pinda Mbali na kufundisha, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na uzalishaji mali katika nyanja za kilimo, mifugo, maliasili na utalii.pia watumishi na wanachuo ushiriki katika mambo mbalimbali ya kijamii kama kuchangia damu,michezo.



*Katika Picha: Baadhi ya wachezaji wa timu ya watumishi wa Kampasi ya Mizengo walipokwenda kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya Idara ya Afya ya Halmashauri ya Mpimbwe. Mchezo uliochezwa katika kata ya Mamba, Halmashauri ya wilaya ya Mpimbwe.*




*Katika Picha ni Timu ya Watumishi wa Idara Afya ya Halmashauri ya Mpimbwe.*



*Mchezo wa draft ulionesha ujuzi wa Prof. Makinda, Naibu Kaimu Rasi wa Utawala, Mipango na Fedha na Dkt. Herman Osca Ntungwa wa Kampasi ya Mizengo Pinda, Mchezo wa bao pia ulishindanishwa, ukiwakutanisha watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda, Mhadhiri Msaidizi Mr. Yahaya na Mr. Godwine Tuloline Mwanzembe.*



*Katika picha: Dkt. Farida Kweka akionesha umahiri wake katika mchezo wa mpira wa pete wakati walipocheza dhidi ya watumishi wa Idara ya Afya wa Halmashauri ya Mpimbwe katika kata ya Mamba, kama sehemu ya kudumisha afya na kuimarisha ujirani mwema.*

## Wahariri

**Mhariri Mtendaji -** Bw. Joseph Ruboha
**Mhariri Mkuu -** Bi. Suzan Magobeko
**Waandishi -** Bw. Edson Kanisa
Prof. Jeremiah Makindara

## Limetolewa na:

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
Kampasi ya Mizengo Pinda
S.L.P 82, Mpanda, Katavi
34 SITALIKE RD
50318 Kibaoni, Mlele
Barua pepe: principalmpc@sua.ac.tz




**YALIYOMO......Uk**

Ujumbe Kutoka Kwa Kaimu Rasi Wa Kampasi ya Mizengo Pinda......01

WAJUMBE WA BODI YA NDAKI......02

UONGOZI WA CHUO......03

Mtambue Mdudu Nyuki na Faida Zake......04

Safari ya Mhitimu wa SUA Kueleke Ujasiriamali wa Bidhaa Zitokanazo na Rasilimali Nyuki......09

SUA Kampasi ya Mizengo Pinda yashiriki vyema kwenye Maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika Mkoani Dodoma na kufungwa na Makamu wa Raisi wa Jamahuri ya Muungano Wa Tanzania Dkt Phipo Mpango tarehe 20 Mei 2024......10

Watafiti na Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kuzitafsiri kwa vitendo tafiti mbalimbali wanazozifanya ili ziwe na maana kwa wananchi......12

Mhe. Dkt. Doto Biteko Atangaza Maagizo Mapya kwa Wizara na Mikoa Kukuza Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi......13

Jinsi Mradi wa Elimu ya Juu Unavyochochea Maendeleo ya SUA Kampasi ya Mizengo Pinda......16

Kaimu Rasi wa Ndaki, Prof. Anna Sikira, Atoa Mwongozo kwa Wanachuo Wapya Kampasi ya Mizengo Pinda......18

MPC-Katika Michezo......19